STANDARD 5 TERM 3 EXAMS 2017, KISWAHILI

Chagua Jibu lifaalo Zaidi kujaza nafa sizilizoachwa wazi

Siku ___1___ Mbweha na Chui walizozana ___2___ nani kati ___3___ alikuwa mzuri ___4___ mwenzake. Chui alijinadi kwa kumwonyesha mbweha moja ___5___ ya jingine madoa ___6___ ngozi ___7___.

Waliendelea kujibizana kwa ___8___ mrefu hadi sungura alipowasili. Sungura akawa kama ___9___ anayesikiliza kesi na kukata kauli. Sungura alionyesha ___10___ yake kwa kutatua shida hiyo.

	A	B	C	D
1.	mmoja	limoja	moja	chache
2.	kuhusu	kama	Kwamba	kwanini
3.	lao	zao	mwao	yao
4.	kuwaliko	kuliko	kumliko	katika
5.	baada	kabla	badala	pengine
6.	iliyoipamba	yaliyoipamba	zilizoipamba	yatakayoipamba
7.	zake	lake	yake	naye
8.	mda	munda	wakati	muda
9.	wakili	askari	hakimu	mshukiwa
10.	ujanja	hekima	heshima	aibu

Penye moshi hapakosi ___11___, chambilacho ___12___. Maisha ___13___ mjini yalionekana kuwateka vijana hawa ___14___ waliishi kwa anasa bila kujali ___15.___

	A	B	C	D
11.	chakula	joto	kuni	moto
12.	wahenga	mababu	walimu	wazee
13.	za	la	ya	kwa
14.	ambaye	ambao	ambako	ambalo
15.	kamwe!	lo!	nani!	hata!

Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa

16. Msimu wa mvua nyingi huitwa
    A. Kipupwe B. kiangazi
    C. mafuriko D. masika

17. Mtoto wa ndege huitwa _____
    A. kifaranga B. kinda
    C. shibli D. kiyoyo

18. Tegua kitendawili hiki:
"Ajenga ingawa hana mikono"
A. ndege B. fundi
C. saa D. nyundo

19. Nomino 'Birika' inapatatikana katika ngeli ya
A. KI — VI B. LI — YA
C. U — U D. I — ZI

20. Andika wingi wa sentensi hii:
Mwiba ulinidunga.
A. Miiba ilinidunga
B. Miiba zilitudunga
C. Miiba ilitudunga
D. Mwiba ilitudunga

21. Kamilisha tashbihi msiri kama _____
A. Kaburi B. serikali
C. shetani D. usiku

22. Tumia kirejeshi "ndi" kukamilisha
Nywele za mtoto _____ zilizokatika
A. Ndizo B. ndio
C. ndiyo D. ndiko

23. Jibu la maamkizi sabalkheri ni _____
A. Alamsiki B.sabalkheri
C. salkheri D. masalkheri

24. Maana ya msemo 'kufa moyo' ni ____
A. aga dunia B.poteza matumaini
C. angamia D.ishiwa nguvu

25. Tumia -enye kujaza pengo
Kuta _____ uchafu zitaoakwa rangi
A. Lenye B. wenye
C. zenye D. penye

26. Andika sentensi hii ukitumia "ki" ya udogo
'Mto umekauka'
A. Jijito limekauka
B. Kamto kamekauka
C. Kijito kimekauka
D. Kimto kimekauka

27. Ukijumlisha nusu na robo utapata
A. Robo tatu B. theluthi mbili
C. robo tatu D. sudusu

28. Sauti gani hapa ni ghuna ?
A. Th B. k C. p D. r

29. Andika tarakimu hii kwa maneno 10,001
A. Elfu kumi na moja
B. Kumi elfu an moja
C. Elfu moja na moja
D. Laki moja na moja

30. Mahali ambapo vitabu huazimwa ili kusoma huitwa aje ?
A. Maabara B. sebuleni
C. maktaba D. zahanati

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 – 40

Mkazi wa mtaa Tuleni katika kaunti ya Masumbuka, Fatima Rashidi mwenye umri wa miaka thelathini na mbili amehukumiwa kifungo cha nje miezi sita, baada ya kupatikana na hatia ta kuiba mtoto mchanga wa wifi yake mwenye umri wa wiki mbili.

Hukumu hiyo imetolewa na hakimu wa mahakama ya wilaya hiyo, Musa Ngaru baada ya kuridhishwa na ushahidi uliokuwa umetolewa na upande wa mashtaka. Kabla ya kutolewa kwa adhabu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea, ambapo aliiomba mahakama imuonee huruma kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza na ana wazazi wanaomtegemea.

Wakili wa serikali, bwana Rabia Ramadhani kwa upande wake aliiomba mahakama kupatia adhabu kali mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na wanawake wengine walio na tabia ya aina hiyo. Hakimu Ngara alimhukumu kifungo cha miezi sita kwa masharti ya kutotenda kosa ndani ya kipindi hicho.

31. Mtoto aliyeibwa alikuwa na umri gani?
A. Miaka miwili B. majuma mawili
C. miezi miwili D. miezi sita

32. Mtu anayetoa hukumu mahakamani anaitwa _____
A. Hakimu B. wakili
C. mahakama D. mshtakiwa

33. Wifi ni _____
A. Mke wa ndugu yako
B. Jirani mwanamke aliyekaribu nawe
C. Mwanamke mwenye tabia ya kuiba watoto.
D. Jina wanaloitana mke wa mtu na ndugu wa kike wa mume wake

34. Mwanamke aliyeiba mtoto anajulikana kwa jina kama _____?
A. Rabia B. Fatuma
C. Ngaru D. Ramadhani

35. Kifungo cha nje ni kifungo cha aina gani ?
A. Ni kifungo ambako uko huru kufanya chochote
B. Ni kifungo unachotumikia ukiwa nje ya gereza na kulala nyumbani kwako
C. Ni kifungo ambacho utaishi nje ya nyumba
D. Ni kifungo ambacho utatumikia ukiwa nje ya nchi.

36. Kwa nini mshtakiwa aliomba kusamehewa?
A. Alidai kwamba kosa lake lilikuwa la kwanza na wazazi wake walimtegemea yeye.
B. Alidai kosa lake lilikuwa dogo
C. Wazazi wake wangetaabika
D. Kwa maana hakimu hakuwa na huruma

37. Kwa nini wakili wa serikali aliiomba mahakama kutoa hukumu kali?
A. Ili iwe funzo kwa watu wote wenye tabia kama hiyo
B. Ili mzazi wa mtoto aliyeibwa aridhike na mahakama itoe funzo kwa wote
C. ili iwe funzo kwa mshtakiwa na wengine wenya nia ya kutenda kitendo kama hicho
D. Kwa sababu hukumu aliyopewa ilikuwa ndogo ikilinganishwa na kosa alilolitenda

38. Mtu anapopatikana na hatia ya jinai na kuhukumiwa hupelekwa _____
A. Mahakamani B. korokoroni
C. kizimbani D. gerezani

39. Kabla ya hukumu kutolewa, mambo haya yote hutendeka isipokuwa _____
A. Mshtakiwa hupewa wakati wa kujitetea
B. Mawakili wa pande zote mbili hutoa maoni yao
C. Mashahidi wote sharti wawe pale wakati wa mshukiwa kuhukumiwa
D. Hakimu husikiza ushahidi wote uliotolewa.

40. Baada ya mshtakiwa kuhukumiwa, alipewa sharti moja kwamba.....
A. Asije akaiba mtoto mwingine tena
B. Asitende kosa jingine anapotumikia kifungo chake
C. Anaweza kulipa faini ikiwa ana pesa
D. Asirudi mahakamani tena.

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50

Kenya ina hali inayowezesha kustawisha aina mbalimbali za matunda. Mazao hayo ni muhimu kwa chakula , biashara, na ni chanzo cha virutubisho vya vitamini na madini ambayo hupatikana kwa wingi kwenye vyakula hivi kuliko kwenye vyakula vingine. Matunda ni tegemeo la mwili katika kupata vitamin na madini mbalimbali yanayohitajika kuulinda mwili kila siku.

Vitamini r a madini yapatikanayo katoka mazao haya hayahifadhiki katika mwili wa binadamu kama vile protini na wanga. Wa hivyo kutokana na umuhimu wake na kutoweza kuhifadhika mwilini ni lazima matunda yajumlishwe kwenye mlo au milo ya kila siku.

Watu wengi hawajatambua umuhimu wa kula matunda. Kuna baadhi ya makabila kwao matunda ni chakula cha mama na watoto tu. Kwa hiyo basi tabia ya kula aina nyingine ya vyakula pasipo kula matunda ni kudhulumu afya ya mwili wako.

Baadhi ya matunda yanayopatikana nchini ni machungwa, maembe, mananasi, mapapai, maparachichi na ndizi. Mapapai ni zao moja kati ya mazao ya matunda yenye vitamini A na madini ya kalsiumu kwa wingi. Maparachichi ni muhimu katika lishe kwani lina mafuta na protini kwa wingi kuliko tunda lingine. Ndizi ni zao moja kati ya mazao ya matunda ambayo huzalishwa kwa wingi katika nchi yetu. Zao hili hutumika kama zao la biashara, chakula na tunda pia.

Vilevile kuna matunda pori au ya asili kama vile ubuyu, ukwaju, embe ng'ong'o, mabungo na kadhalika.

41. Ni hali gani inayoifanya Kenya kuzalisha matunda ya aina nyingi?
    A. Hali ya hewa
    B. Mchanga wenye rotuba
    C. Wakulima hodari
    D. Elimu nyingi

42. Kati ya matunda haya, ni tunda gani ambalo ni la porini
    A. Parachichi B. Nanasi
    C. Ukwaju D. Embe

43. Ni zao gani ambalo hutumika kama chakula, tunda na pia biashara?
    A. Embe ng'ong'o B. Papai
    C. Chungwa D. Ndizi

44. Ni aina gani ya matunda ambayo yana mafuta kwa wingi?
    A. Maembe B. Maparachichi
    C. Mapesheni D. Mapapi

45. Mbona watu wengi hawali matunda?
    A. Matunda ni ghali mno
    B. Hawapendi kula matunda
    C. Baadhi yao huona matunda ni chakula cha mama na watoto
    D. Matunda husababisha magonjwa mengi

46. Kwa nini ni vyema kula matunda kila siku ikilinganishwa na vyakula vingine?
    A. Kwa kuwa vitamini na madini yapatikanayo katika mazao haya hayahifadhiki katika mwili.
    B. Matunda ni mengi sana humu nchini
    C. Ni rahisi kutayarisha au kuandaa matunda
    D. Matunda yana bei nafuu

47. Matunda yote kwa jumla yanapatikana kuwa na _____
    A. Protini B. kalsiumu
    C. Vitamini A D. Virutubisho

48. Ni vizuri kula matunda mara nyingi chambilecho wahenga;
    A. Siku za mwizi ni arobaine
    B. Bendera hufuata upepo
    C. Kinga ni bora kuliko tiba
    D. Ajali haina kinga

49. Miti hii yote ni ya matunda ila _____
    A. mpera B. mlimau
    C. mchungwa D. mpunga

50. Kichwa bora kwa taarifa hii ni?
    A. Umuhimu wa matunda katika miili yetu
    B. Kenya inaongoza katika zao la matunda
    C. Aina mbalimbali za matunda
    D. Ukosefu wa matunda katika jamii

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com